

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam  
19 Julai 2008**

**Waliohudhuria**

Ally Athuman Jumbe  
Ally Saidi Mwishehe  
Aseli Wilison  
Bashiri Rashidi  
Dominata Rwechungura  
Edgar R Paulo  
Elaine Baker  
Filbert Mbecha  
Frank Peter Rwechungura  
Husein Hamza Hamisi  
Juma Ali Salehe Jongo  
Juma Ayoubu Ally  
Jumanne Idd Selemani  
Kibwana Mohammad Msiga  
Mussa Alex  
Ramadhani Rajabu Nyengo  
Sosthenes C Amlima

**Mradi wa Usalama Barabarani - Wamba Memorial Fund**

Wakati wa wiki Elaine alichapa sahihi kwenye mwongozo kama Dominata na Filbert walivyoweka, na aliprint na kutoa photocopy kwa washiriki.

Jumatatu Elaine na Juma walienda Chuo cha Usafirishaji na alhamisi Juma alienda tena. Bwana Sempoli alitusaidia kutayarisha darasa na chakula cha washiriki. Chai ya asubuhi na chakula cha mchana itakuwa Tsh 1,600 kwa mtu. Juma atalipa Tsh 40,000 advance kwa siku moja.

Mwalimu moja kutoka Kigamboni Secondary School, walimu wawili kutoka Msongole, wawakilishi wawili wa HUWATA, wawakilishi watatu wa chuo cha usafirishaji, na wanachama 17 wa UWABA watashiriki, ambayo ni washiriki 25 na Andrew. Tuliongea kuhusu kupunguza kiasi cha washiriki lakini mwishoni tulikubali kwamba kila mtu aliyejiandikisha ataruhusu kushiriki.

Andrew anafika saa moja na nusu jioni jumapili. Anakuja na baisikeli yake. Elaine atampokea na teksi na atakaa kwake Kigamboni.

Elaine ataandaa documents kuleta kwenye mikutano alhamisi. TANROADS walimpigia simu Mejah kuuliza kuhusu mkutano na Andrew.

Elaine pia ataandaa vyeti vya kuhudhuria kwa ajili ya washiriki wa kozi.

**Mambo ya hela**

Elaine na Juma walienda benki na walichukua Tsh 1,000,000 ili kuwa na hela karibu kwa ajili ya kozi, na kila mmoja alibaki na Tsh 500,000. Elaine alitumia Tsh 22,400 kwa ajili ya photocopying. Juma alipokea kodi ya guta ya wiki mbili Tsh 14,000. Elaine sasa ana Tsh 477,600 na Juma ana Tsh 579,950 ya hela ya UWABA.

**Mambo ya ofisi**

Mejah alitumia message kusema lazima atapaka rangi kwenye ofisi mpya kabla ya tarehe 1 Augusti.

**Mambo mengine**

UWABA tulipokea email kutoka mpanda baisikeli wa Dar es Salaam anaitwa Amar ambaye anapenda kujiunga na UWABA.